# JIMBO KATOLIKI LA NJOMBE

## SHULE YA SEKONDARI UMAWANJO BOYS'

**S. L. P 54,**
**NJOMBE,**
**TANZANIA,**
**AFRIKA MASHARIKI.**

**Barua pepe:** umawanjoboys@gmail.com

**Simu No.** **+255-748-354-813 shule**
**+255-762-251-241 makamu**
**+255-756-047-671 mtaaluma**
**+255-769-765-361 mhasibu**

---

**MKUU WA SHULE**
**Simu: +255-769-392-240**

**Ndugu Mzazi/ Mlezi wa …………………………………………………**
**S. L. P ……………………………………**

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI UMAWANJO BOYS'**

Husika na kichwa cha habari chajieleza hapo juu. Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari tajwa hapo juu. Shule ipo katika kijiji cha **Lugarawa**, Kata ya **Lugarawa**, Wilaya ya **Ludewa** Mkoa wa **Njombe**. Kutoka **Njombe mjini hadi shuleni ni KM 105**.

Shule itafungua tarehe **03/10/2026** tayari kwa kuanza masomo ya awali kwa kidato cha kwanza (Pre form one course). Unatakiwa kufika kabla ya saa 12.00 jioni.

**Unapofika shuleni fika na**;

i. Taarifa ya daktari juu ya afya yako.
ii. Mahitaji yote yanayokuhusu kadri ya maelekezo.
iii. **Bima ya NHIF,** kama hana afike na **Tsh 50400/- ni lazima**

Nakutakia maandalizi mema, karibu sana katika shule hii. (Umawanjo Boy's Secondary School)

……………………………………
**FRANSISCO G. KAYOMBO**
**Simu: +255-769-392-240**
**MKUU WA SHULE**

**NB**: Mwanafunzi hatapokelewa kama hajakamilisha **MAHITAJI.**

Motto wa Shule ni *Elimu na Malezi Bora*.

Karibu sana UMAWANJO BOYS', "DIVISION ONE FOR ALL"

# FOMU YA KUJIUNGA

1. **ADA:** Ada zetu ni **Tsh 2,200,000/=** (Milioni Mbili na Laki Mbili), Italipwa kwa awamu **NNE.** Malipo haya yataanza mwezi Januari 2027. Yaani **Tsh550, 000/-** kila awamu. Malipo kwenye **CRDB**
2. **SARE** : Mwanafunzi aje na sare aliyokuwa anavaa shuleni na suluari nyeusi moja na Track suti Nyekundu yenye michilizi myeupe **(02),** pulneki nyeusi (kwaajili ya kuvaa wakiwa pre- form one)
3. Malipo ya masomo ya Maandalizi ya Kidato cha Kwanza (Pre Form one) ni **Tsh 200,000/=** (Zilipwe kwa mhasibu wa shule na utapewa risiti).
4. Michango kwa ajili ya mitihani itakayokuwa inafanyika wakati wa mafunzo ya pre- form one – **20,000**/=
5. Mchango kwa ajili ya kushiriki mahafali ya kaka zao **Tsh 15,000/-** italipwa kwa mhasibu wa shule na utapewa risiti.
6. **SARE ZA KIDATO CHA KWANZA**: Malipo ya sare kwa ajili ya kidato cha kwanza ni Tsh **230,000**/= Sare zote zitapatikana shuleni. Sare itakuwa ni suruali mbili za darasani, suruali mbili shamba dress, sweta moja, form six tatu na jezi kamili full jersey moja. Malipo yafanyike kupitia **bank ya mkombozi, fika na risiti unaporipoti pre-form one.**
7. **Mchango wa Maabara** ni **Tsh100,000/=** Malipo yafanyike januari 2027 **bank ya mkombozi**
8. **Ukarabati tsh 50,000/- malipo ni januari 2027 kwenye bank ya mkombozi**
9. **Malipo ya mitihani akiwa kidato cha kwanza tsh 50,000/-** malipo ni januari 2027 kwenye bank ya mkombozi.

**NB; AKAUNTI (ACOUNT) ZA BANKI— CRDB 0150349985100 kwa ajili ya ADA/KARO tu**

**----MKOMBOZI 01011512621501 kwa ajili ya michango tu**

10. **MAHITAJI HAYA MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO. MAHITAJI YANAPATIKANA KATIKA DUKA LA SHULE PIA.**

- Daftari, aje na daftari **saba kaunta (counter books) quire two** kwa ajili ya pre-form one course
- Kalamu za bluu na penseli
- Mkebe (Mathematical set) na Kamusi kubwa (kiingereza- Kiswahili)
- Blanketi mbili (2)
- Shuka za pinki nne (4)
- Taulo
- Godoro 2 $^1/_2$" , mto na foronya zake
- Neti- kwa ajili ya mbu
- Gumboot jozi moja (1)
- Ndoo lita 10 (kuogea na kufanya usafi binafsi) ▪ Vifaa vya mezani – kontena, Kikombe. **Vyote viwe vya rangi ya bluu.**
- Soksi nyeusi jozi nne (4)
- Nguo za ndani
- Rimu moja NO: 01 kwa walio Njombe na Makambako inapatikana MLOMBOJI STATIONARY.
- Tranka moja (1) na kufuli.
- Raba jozi mbili (02) za michezo na saa ya kawaida
- Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili (2) vyenye kamba
- Mkanda mweusi wa ngozi
- Leso za kutosha
- Dawa ya meno, Mswaki na Kitana
- Fulana za kutanguliza ndani za kutosha (Nyeupe)
- Jembe moja na mpini wake

Tunaomba vyote viwekewe alama kwa kuandika majina ya mwanafunzi.Ili kuepusha usumbufu wa usafirishaji, mahitaji haya yote yanapatikana hapa shuleni kwa bei nafuu.

**UMAWANJO BOYS' SECONDARY SCHOOL,**
**DIOCESE OF NJOMBE,**
**P.O. BOX 54, NJOMBE.**

# MEDICAL CERTIFICATE

Name…………………………………………………………………………..

**General Condition of Health**

1. Skin…………………………………………………………………
2. Head…………………………………………………………………
    i. Eyes………………………………………………… ii. Ears…………………………………………………….
    iii. Mouth……………………………………………………
3. Chest………………………………………………………………..
    i. X-ray…………………………………………………….. ii. Lungs……………………………………………………. iii. Heart…………………………………………………..
    iv. Abdomen……………………………………………………
4. Extremities………………………………………………………….
5. Nervous system………………………………………………………..

Laboratory Findings

Blood: Hb……………………Stool…………………Blood group……………

Ery ……………………Urine ………………………………………

Leuco……………………………..V.D………………………………

SICKLE CELL TEST

E S R

REMARKS

……………………………………………………………………

……………………………………………………………………

……………………………………………………………………

………………………………

DOCTOR IN CHARGE

**NB: Please don't forge**

**JIMBO KATOLIKI LA NJOMBE**

## SHULE YA SEKONDARI UMAWANJO BOYS’

### SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE

**MWANAFUNZI ALIE TAYARI KUJIUNGA NA SHULE HII AWE TAYARI KUZINGATIE SHERIA, MIONGOZO NA TARATIBU ZIFUATAZO**

1. Kila mwanafunzi anatakiwa kuvaa kwa namna ya kufaa nguo rasmi za shule darasani na popote anapokwenda nje ya Shule
2. Mwanafunzi anapaswa kuwa katika mazingira ya Shule daima. Kibali cha kutoka nje ya shule kitatolewa na **Mkuu wa Shule au Makamu wake** kwa shida maalum.
3. Ukosefu wa nidhamu wa aina yoyote hautavumilika.
4. Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu viongozi wote kuanzia mwanafunzi hadi Mkuu wa Shule.
5. **Kazi ni sehemu ya Elimu** kwa hiyo kila mwanafunzi lazima ashiriki kikamailifu katika kazi za elimu ya kujitegemea na nyingine za kujenga Taifa.
6. Mwanafunzi anapaswa kuheshimu wimbo wa **TAIFA NA SHULE.**
7. Mwanafunzi awahi kila anapoitwa na kusikia mlio wa kengele.
8. Mwanafunzi awepo darasani na ajifunze kimya bila kelele.
9. Hairuhusiwi kupeleka chakula cha aina yoyote bwenini, chakula chote kiliwe katika bwalo la chakula.
10. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi yeyote kuletewa chakula au kujipikia chakula.
11. Matatizo madogomadogo yaanze kushughulikiwa kwanza na viongozi wa wanafunzi au walimu wa zamu kabla ya kuyafikisha kwa Mkuu wa Shule au Makamu Mkuu wa Shule.
12. Hairuhusiwi kutumia lugha chafu **(matusi)** au kupigana.
13. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa muungwana, mtiifu,mwadilifu na mwajibikaji.
14. Utoro hautahurumiwa kamwe. Mtoro wa shule anakuwa amejifukuza mwenyewe.
15. Kosa lolote la jinai halitavumilika.
16. Kila mwanafunzi aheshimu na kuthamini imani ya dini yake na ya mwenzie.
17. **Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki au kutumia simu yeyote au kuwa na kifaa chochote kinachotumika katika simu pindi awapo shuleni, bila ya ruhusa ya Mkuu wa shule au Makamu wake.**
18. Kila mmoja anapaswa kuwa mlinzi wa mali zake, za mwenzake na za Shule. Uharibifu wa mali hizo hapo juu ni kosa kubwa. Mali iliyoharibiwa itafidiwa na muhusika/wahusika mara mbili yake
19. Silaha ya aina yoyote hairuhusiwi
20. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi kutembea peke yake, Kila mtembeapo ndani au nje ya mazingira ya Shule mnatakiwa kuwa watatu au zaidi.
21. Hairuhusiwi kuanzisha, kukubali au kushiriki **MGOMO** wa aina yoyote ile. Matatizo ya wanafunzi yawasilishwe kwa Uongozi wa wanafunzi, Walimu wa Idara, Mkuu wa Shule au Makamu wake.

**IWAPO MWANAFUNZI ATAPATIKANA NA MAKOSA YAFUATAYO:-**

1. Utoro wa aina yoyote
2. Wizi
3. Uasherati
4. Kupigana na kutukana,kutoa maneno ya kashfa .
5. Kuvuta bangi au kutumia madawa ya kulevya
6. Kulewa (Kutumia pombe)
7. Kuanzisha, kukubali au kushiriki **MGOMO**
8. Kuimiliki, kuwa na kifaa cha simu au kutumia simu bila ya ruhusa ya Mkuu wa Shule au Makamu wake

**ATAONDOLEWA SHULENI MARA MOJA BILA KUPINDISHA SHERIA KABISA.**